



Viwango vya Kilimohai Afrika Mashariki

Uchakataji na Uhifadhi wa bidhaa za kilimohai



**Imeandaliwa na Shirika la Kilimohai Tanzania- TOAM,
2026**



In cooperation with



1 Jinsi ya kutunza ubora wa bidhaa za kilimohai

- Pokea malighafi kutoka kwa wazalishaji waliothibitishwa wa kilimohai



- Fanya uchambuzi, usafi, upangaji na ukaushaji kwa uangalifu ili kulinda ubora wa bidhaa.
- Tumia vifaa tofauti au safisha vifaa vizuri kati ya matumizi ili kuzuia uchafuzi.
- Safisha vyombo, vifaa na sehemu za kazi kabla ya matumizi hata kama vinatumika kwa bidhaa za kilimohai.

- Weka kumbukumbu za malighafi zinazolingia, uchakataji, uhifadhi, usafirishaji, mauzo ya bidhaa ili kuhakikisha ufuatiliaji wa bidhaa kutoka kwa mzalishaji hadi kwa mlaji.



- Tumia maji safi na salama wakati wa uchakataji.
- Linda bidhaa dhidi ya uchafuzi kutoka mazingira yanayozunguka eneo la uchakataji.
- Uchakataji ufanyike kwa kutumia mbinu za kimakanika, kiasili, kibaiolojia, au vimeng'anya vya asili ili kuhifadhi ubora wa asili wa bidhaa.
- Njia za asili kama kukausha, kuvundika, kufukiza moshi, kusaga, kukamua zinashauriwa.
- Epuka matumizi ya kemikali na rangi bandia.
- Usitumie kemikali kufanya bidhaa zionekane mpya au bora zaidi.

2. Mahitaji ya Jumla ya Uchakataji wa Bidhaa za kilimohai chini ya EAOPS

2.1 Kudumisha uhalisia wa kilimohai

- Uchakataji wa bidhaa za kilimohai unapaswa kulinda uhalisia wa bidhaa katika hatua zote za uvunaji, uhifadhi, uchakataji na usafirishaji.
- Usichanganye bidhaa za kilimohai na zisizo za kilimohai. Zitenge na weka alama
- Kila bidhaa ya kilimohai iweze kufuatiliwa kutoka kwa mzalishaji hadi kwa mlaji
- Bidhaa za kilimohai zisafirishwe kwa namna inayozuia uchafuzi au kuchanganywa na bidhaa zisizo za kilimohai.
- Vyombo vya usafirishaji viwe safi na visitumike kusafirisha kemikali au bidhaa zinazoweza kuchafua bidhaa za kilimohai.



3. Mahitaji ya Jumla ya Uchakataji wa Bidhaa za kilimohai chini ya EAOPS ...

2.2 Matumizi ya viambata vya kilimohai

- Bidhaa zilizochakatwa zinapaswa kutengenezwa kwa kutumia viambato vya kilimohai.
- Usichanganye viambato vya kilimohai na visivyo vya kilimohai hata kama vinafanana.
- Maji na chumvi huruhusiwa lakini havihesabiwi katika asilimia ya viambato vya kilimohai.
- Usitumie viambato au malighafi zilizobadilishwa vinasaba (GMO).




Itakuwaje kama viambata vya kilimohai havipatikani?

- Katika hali maalum, viambato visivyo vya kilimohai vinaweza kutumika ikiwa havijabadilishwa vinasaba, havipatikani katika eneo husika na idhini imetolewa na chombo cha udhibiti.

4. Uchakataji wa bidhaa za kilimohai

- Tumia njia rahisi za asili kama kukausha, kusaga, na kuvundika.
- Epuka matibabu ya kemikali au bandia.



- Safisha vifaa, filters na trays za kukaushia mara kwa mara.
- Tumia vifaa salama kwa chakula ambavyo haviwezi kuchafua bidhaa za kilimohai

5. Njia za udhibiti wa wadudu na magonjwa

- Weka eneo la uchakataji safi wakati wote.
- Tumia njia za kuzuia kwanza kwa kuhakikisha usafi.



Tumia njia za asili na kimwili kudhibiti wadudu kama mitego, mwanga, na njia za asili za kufukuza wadudu

- Usitumie fumigation ya kemikali, dawa za kemikali au mionzi kwa sababu huharibu uhalisia wa bidhaa za kilimohai.
- Weka kumbukumbu za shughuli zote za kudhibiti wadudu.
- Hifadhi bidhaa sehemu safi, kavu, zenye hewa ya kutosha na mbali na kemikali na wadudu
- Wafanyakazi wanapaswa kudumisha usafi binafsi wakati wa kushughulikia bidhaa za kilimohai.



6. Ufungashaji

- Tumia vifungashio safi, salama na rafiki kwa mazingira ili kulinda bidhaa na mazingira.
- Chagua vifaa vinavyoweza kuoza, kutumika tena, au kurejelewa kama karatasi, katani, glasi au plastiki salama kwa chakula
- Vifungashio visitumie kemikali, vihifadhi au dawa zinazoweza kuathiri ubora wa bidhaa.
- Baada ya kutumia kemikali za usafi au usafishaji, hakikisha muda wa kutosha unapita kabla bidhaa za kilimohai kugusa sehemu hiyo ili kuzuia mabaki ya kemikali kwenye bidhaa

7. Uwekaji wa Lebo

Bidhaa za kilimohai lazima ziwe na lebo zinazoonesha taafifa zifuatazo:

- Taarifa za uthibitishaji
- Viambato vya bidhaa
- Asilimia ya viambato vya kilimohai
- Bidhaa yenye asilimia 95-100 ya viambato vya kilimohai inaweza kuandikwa "ORGANIC".
- Bidhaa yenye asilimia 70-94.9 inaweza kuandikwa:
- "Made with organic" pamoja na kuonesha asilimia husika.
- Ikiwa kiwango cha viambato vya kilimohai ni chini ya 70%, neno "ORGANIC" halipaswi kutumika kwenye lebo.
- Usitumie lebo, picha au taarifa zinazoweza kumpotosha mlaji kuhusu bidhaa za kilimohai.

Kuhusu kipeperushi hiki

Kipeperushi hiki kinaelezea mahitaji muhimu ya uchakataji na uhifadhi wa bidhaa za kilimohai kwa kuzingatia viwango vya East African Organic Products Standards (EAOPS). Kiwango hiki kilipitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2007 na kufanyiwa maboresho kila baada ya miaka mitano hivyo kuwa kiwango rasmi kwa Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Kipeperushi hiki rahisi kimeandaliwa na Mwamvuli wa Kilimohai Tanzania (Tanzania Organic Agriculture Movement -TOAM) kupitia Mradi wa Kitovu cha Maarifa ya Kilimo Ikolojia Hai Afrika Mashariki (Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology in East Africa – KHEA).

Mradi huu unalenga kuandaa, usambazaji wa maarifa na matumizi ya kilimo Ikolojia hai katika Afrika Mashariki. Unafadhiliwa na GIZ kupitia Biovision African Trust (BvAT)

Unaweza kupata maarifa kama haya na mengine mengi kutoka Tanzania na afrika kwa ujumla kwa kutembelea tovuti: <https://khea-africa.org/> na <https://kcoa-africa.org/>
KHEA Website

Mawasiliano

 info@kilimohai.org

 +255 744 134 999

Machapisho mengine katika mfululizo huu

- Uzalishaji wa Mazao
- Uzalishaji wa Mifugo
- Uzalishaji wa Viumbe Maji
- Ufugaji wa Nyuki